**SHERIA YA KUANZISHA BARAZA LA TAIFA LA BIASHARA NA KUWEKA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**


**SEHEMU YA KWANZA**
**VIFUNGU VYA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Matumizi
3. Ufafanuzi.

**SEHEMU YA PILI**
**UANZISHWAJI WA BARAZA LA TAIFA LA BIASHARA ZANZIBAR**

4. Uanzishwaji wa Baraza.
5. Mhuri wa Baraza.
6. Muundo wa Baraza.
7. Uteuzi wa Wajumbe wa Baraza.
8. Malengo ya Baraza.
9. Kazi za Baraza.
10. Mkutano wa Baraza.
11. Uteuzi wa Katibu Mtendaji.
12. Majukumu ya Katibu Mtendaji.
13. Wafanyakazi wa Baraza.

## SEHEMU YA TATU
## UANZISHWAJI NA MUUNDO WA KAMATI TENDAJI YA BARAZA


14. Uanzishwaji wa Kamati Tendaji.

15. Muundo wa Kamati Tendaji.

16. Kazi za Kamati Tendaji.

17. Mkutano wa Kamati Tendaji.


## SEHEMU YA NNE
## UANZISHWAJI WA KAMATI ZA BARAZA


18. Kamati za Baraza.

19. Kumualika mtu.

20. Kazi za Kamati.


## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YANAYOHUSIANA NA MABARAZA YA MIKOA


21. Muundo wa Baraza la Mkoa.

22. Kazi za Baraza la Mkoa.

23. Wajibu wa Baraza la Mkoa.


## SEHEMU YA SITA
## UANZISHWAJI WA JUKWAA LA BIASHARA


24. Kuanzishwa kwa Jukwaa la Biashara.


## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI YA FEDHA


25. Vyanzo vya fedha.

26. Makadirio ya Mwaka.

27. Hesabu na Ukaguzi.

## SEHEMU YA NANE
## MASHARTI MENGINEYO

28. Kanuni.

29. Kufuta na kubakiza.

**JADWELI LA KWANZA.**

**JADWELI LA PILI.**

**JADWELI LA TATU.**

**SHERIA NAMBA 10 YA 2017**

**NIMESAINI**

Alhemis

**{DR. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

1st November, 2017

# SHERIA YA KUANZISHA BARAZA LA TAIFA LA BIASHARA ZANZIBAR NA KUWEKA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## VIFUNGU VYA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Baraza la Taifa la Biashara Zanzibar ya 2017 na itaanza kutumika baada ya kusainiwa na Rais.

Matumizi.

**2.** Sheria hii itatumika kwa Sekta ya Umma na Sekta binafsi kwa ajili ya Jukwaa la biashara na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Ufafanuzi.

**3.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Baraza la Taifa la Biashara Zanzibar;

"Mwenyekiti wa Baraza" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Jumuiya" maana yake ni Jumuiya ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Wakulima Zanzibar;

"Kamati" maana yake ni Kamati za Baraza zilizoanzishwa chini ya kifungu cha 18 cha Sheria hii;

"Baraza" maana yake ni Baraza lililoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria hii;

"Katibu Mtendaji" maana yake ni Katibu Mtendaji wa Baraza aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 11 (1) cha Sheria hii;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Biashara;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Kamati Tendaji" maana yake ni Kamati Tendaji iliyoanzishwa chini ya Kifungu cha 14 cha Sheria hii.

## SEHEMU YA PILI
## UANZISHWAJI WA BARAZA LA TAIFA LA BIASHARA ZANZIBAR

Uanzishwaji wa Baraza.

**4.**-(1) Kunaanzishwa Baraza litakalojulikana kama Baraza la Taifa la Biashara Zanzibar kwa ufupi litajulikana kama ZNBC.

(2) Baraza litakuwa ni jukwaa la majadiliano ya kibiashara baina ya sekta ya umma na sekta binafsi.

Muhuri wa Baraza.

**5.**-(1) Kutakuwa na Muhuri wa Baraza ambao umbo na ukubwa wake utapendekezwa na Kamati Tendaji na kuamuliwa na Baraza.

(2) Matumizi ya Muhuri wa Baraza juu ya nyaraka yoyote yatathibitishwa na saini ya Katibu Mtendaji au Afisa mwengine yoyote wa Baraza aliyeidhinishwa na Katibu Mtendaji.

(3) Nyaraka yoyote itakayotolewa na Baraza ili ijulikane kuwa ni hati rasmi iliyotolewa na Baraza itatakiwa iwe imepigwa muhuri wa Baraza na imethibitishwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, itachukuliwa kuwa ni hati rasmi ya Baraza na itapokelewa kama ushahidi bila uthibitisho mwengine wowote.

Muundo wa Baraza.

**6.**-(1) Baraza litajumuisha wajumbe wafuatao:

(a) Rais ambaye atakuwa Mwenyekiti;

(b) Mawaziri kutoka Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; na

(c) Wajumbe wasiozidi kumi na mbili kutoka sekta binafsi;

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) (b) na (c) cha kifungu hiki, uwiano wa Wajumbe wa Baraza kutoka Sekta ya Umma na sekta binafsi utakuwa sawa.

(3) Mwenyekiti anaweza kumualika mtu yeyote mwenye weledi kutoka sekta ya umma au sekta binafsi kuhudhuria mkutano wa Baraza ili kutoa mchango kutokana na ujuzi wake kama Mwenyekiti atakapoona inahitajika.

Uteuzi wa wajumbe wa Baraza.

**7.**-(1) Mwenyekiti ana uwezo wa kuteua wajumbe wa Baraza kama ifuatavyo:

(a) Mawaziri kutoka Wizara tofauti kama atakavyoona inafaa; na

(b) Wakuu wa jumuiya za sekta binafsi ambao watateuliwa kutoka Jumuiya ya Wafanyabiashara, Viwanda na Wakulima na wajumbe wengine wasiokuwa wanachama wa Jumuiya hii.

(2) Katika kuteua wajumbe chini ya kifungu kidogo cha (1) (b) cha kifungu hiki, Rais atalazimika kushauriana na Jumuiya.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Rais atazingatia jinsia katika kuteua wajumbe kutoka sekta binafsi.

(4) Wajumbe kutoka sekta binafsi watatoka sekta mbalimbali ikijumuisha Biashara, Fedha, Viwanda, Utalii, Kilimo na Uvuvi, Uchimbaji Madini, Usafiri na Mawasiliano, Elimu, Afya, Ujenzi na ufundi na sekta nyengine za biashara.

(5) Mwenyekiti wa Baraza baada ya kupokea mapendekezo na kujadiliana na sekta binafsi, anaweza kumuondoa mjumbe na kujaza nafasi kwa mjumbe yeyote kutoka sekta binafsi.

Malengo ya Baraza.

**8.** Baraza la Taifa la Biashara Zanzibar lina malengo yafuatayo:

(a) kuandaa mikutano au majadiliano baina ya sekta za Umma na sekta Binafsi kwa dhamira ya kupata muafaka na uwelewa juu ya mambo ya msingi yanayohusiana na usimamizi na ukuaji wa uchumi;

(b) kuzidisha ukuaji wa uchumi kwa lengo la kupunguza umaskini na kuendeleza maendeleo endelevu;

(c) kutathmini kipindi baada ya kipindi, maendeleo ya mazingira ya kibiashara ya ndani na nje ya nchi, changamoto, na fursa zake kwa lengo la kupata suluhisho;

(d) kubadilishana uzoefu juu ya mazingira yaliyopo ya uendeshaji na usimamizi wa biashara kwa lengo la kuimarisha utendaji mzuri wa biashara na utoaji wa huduma;

(e) kutathmini na kupendekeza uimarishaji wa mazingira bora ya kibiashara ambayo yatavutia uwekezaji na ushindani wa kibiashara; na

(f) kuzingatia jambo jengine lolote ambalo litapelekea Baraza la Taifa la Biashara Zanzibar kufikia malengo yake.

Kazi za Baraza.

**9.** Kazi za Baraza zitakuwa ni:

(a) kukuza mashirikiano ya sekta ya umma na sekta binafsi;

(b) kuweka utaratibu wa majadiliano ya kibiashara baina ya sekta ya umma na sekta binafsi;

(c) kuyapitia mambo yanayoanzia katika mikutano au majadiliano ya Jukwaa yanayohusiana na maendeleo ya kiuchumi na kushauri njia sahihi za utatuaji kwa utekelezaji kwa sekta husika;

(d) kufanya au kupelekea kufanywa utafiti juu ya sera za maendeleo ya kijamii na kiuchumi kama Baraza litakavyoona inafaa;

(e) kupitia utekelezaji wa maazimio ya Baraza kwa sekta inayohusika;

(f) kupokea, kupitia na kutoa mapendekezo juu ya sera, tafiti, taarifa au mapendekezo yaliyowasilishwa kwenye Baraza na sekta husika yanayohusiana na biashara na maendeleo ya kiuchumi;

(g) kuweka malengo pamoja na muda wa utekelezaji wake kwa utekelezaji wa miongozo, maamuzi au maazimio ya Baraza;

(h) kusimamia na kutathmini utekelezaji wa kazi za Baraza;

(i) kupokea na kuipitia taarifa ya utekelezaji ya mwaka ya Baraza na kutoa muongozo;

(j) kuwa na uhusiano au ushirikiano na Mabaraza mengine ya biashara nje ya Zanzibar kwa lengo la kutafuta ujuzi na kubadilishana taarifa;

(k) kuanzisha Kamati endapo itahitajika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za Baraza;

(l) kupokea taarifa ya utekelezaji kutoka Baraza la Mkoa kwa ajili ya kuiidhinisha; na

(m) kufanya kazi nyengine yoyote kwa madhumuni ya kukuza mazingira ya biashara na maendeleo ya uchumi.

(2) Baraza linaweza ikiwa litaona inafaa kwa utekelezaji mzuri wa kazi zake kukasimu baadhi ya kazi zake kwa Kamati au Katibu Mtendaji au Baraza la Mkoa kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi za Baraza.

Mkutano wa Baraza.

**10.** Mkutano wa Baraza, akidi na maazimio yatakuwa kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Kwanza la Sheria hii.

Uteuzi wa Katibu Mtendaji.

**11.**-(1) Kutakuwa na Katibu Mtendaji wa Baraza ambae atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Katibu Mtendaji ikiwa ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya utawala wa umma, usimamizi wa biashara, sheria, uchumi au fani nyengine zinazofanana na hizo kutoka chuo kinachotambulika na uzoefu wa kazi wa angalau miaka mitano.

(3) Katibu Mtendaji atakuwa anawajibika katika kutekeleza majukumu ya kazi zake kama atakavyoelekezwa na Baraza au Kamati Tendaji.

Majukumu ya Katibu Mtendaji.

**12.**-(1) Kwa madhumuni ya Sheria hii, Katibu Mtendaji atakuwa na jukumu la kusimamia na kuratibu mambo yote yanayohusiana na uongozi na shughuli za kila siku za Baraza.

(2) Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Katibu Mtendaji atatekeleza majukumu yafuatayo:

(a) kutekeleza kazi za kila siku za Baraza;

(b) kuandaa na kuweka kumbukumbu za vikao vya Baraza pamoja na Kamati zake;

(c) kutayarisha ajenda zinazotakiwa kujadiliwa katika vikao vya Baraza, Kamati Tendaji na Kamati mbalimbali za Baraza;

(d) kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya Baraza;

(e) kuratibu shughuli za Mabaraza ya Mikoa;

(f) kutayarisha bajeti ya kila mwaka ya Baraza na kuiwasilisha kwa Kamati Tendaji kwa ajili ya kuthibitishwa;

(g) kuandaa mpango mkakati wa kibiashara wa Baraza;

(h) kutayarisha taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa kazi za Baraza; na

(i) kufanya kazi nyengine yoyote atakayoelekezwa na Baraza au Kamati Tendaji.

(2) Katika kutekeleza kazi zilizoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Katibu Mtendaji atakuwa chini ya usimamizi na miongozo ya Waziri.

Wafanyakazi wa Baraza.

**13.**-(1) Katibu Mtendaji baada ya idhini ya Kamati Tendaji, anaweza kuajiri wafanyakazi kwa idadi ambayo ataona inafaa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Baraza kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

(2) Wafanyakazi walioajiriwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, watakuwa chini ya udhibiti na usimamizi wa Katibu Mtendaji.

## SEHEMU YA TATU
## UANZISHWAJI NA MUUNDO WA KAMATI TENDAJI YA BARAZA

Uanzishwaji wa Kamati Tendaji.

**14.** Kutakuwa na Kamati Tendaji ya Baraza.

Muundo wa Kamati Tendaji.

**15.**-(1) Kamati Tendaji itajumuisha wajumbe kumi ambao watakuwa na uwakilishi sawa kutoka sekta ya umma na sekta binafsi kama ifuatavyo:

(a) Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati Tendaji;

(b) Mwenyekiti mwenza ambaye atateuliwa na Kamati Tendaji kutoka miongoni mwa wajumbe wa sekta binafsi;

(c) Wajumbe kutoka sekta ya umma watakaoteuliwa na Katibu Mkuu Kiongozi kama atakavyoona inafaa; na

(d) Wajumbe kutoka sekta binafsi watakuwa ni maafisa waandamizi watakaowakilisha jumuiya zao na watatoka katika Jumuiya, chama cha waajiri, wawekezaji wa utalii, usafirishaji wa bahari na jumuiya zisizokuwa za kiserikali.

(2) Katika kuteua wajumbe kutoka sekta binafsi, Jumuiya ya Wafanyabiashara na jumuiya nyengine ambazo si wanachama wa Jumuiya ya Wafanyabiashara watawasilisha majina wanayoyapendekeza kwa Katibu Mkuu Kiongozi kwa ajili ya uteuzi.

(3) Katibu Mtendaji atakuwa katibu wa Kamati Tendaji.

(4) Bila kuathiri muundo wa Kamati Tendaji, wajumbe kutoka sekta binafsi wanaweza kubadilishwa na Kamati Tendaji kama itakavyoona inafaa.

Kazi za kamati Tendaji.

**16.** Kazi za Kamati Tendaji zitakuwa ni:

(a) kuandaa Mikutano ya Baraza;

(b) kuandaa ajenda za mkutano wa Baraza;

(c) kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo na maazimio ya Baraza;

(d) kuangalia kazi za Katibu Mtendaji wa Baraza kwa ajili ya kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yamefikiwa;

(e) kuandaa utaratibu na itifaki kwa ajili ya kushughulika na kufikiwa kwa maazimio na makubaliano ya Baraza ikijumuisha uratibu na utekelezaji wa maazimio ya Baraza;

(f) kusaidia kufanyika kwa vikao vya Kamati za Baraza;

(g) kuthibitisha na kuidhinisha bajeti ya mwaka, mpango kazi na masuala ya ajira na kuwasilisha kwa Waziri;

(h) kurahisisha utekelezaji wa kazi za Baraza;

(i) kusimamia uongozi na utawala wa Baraza;

(j) kuanzisha muundo wa taasisi na utaratibu wa kutekeleza kazi za Baraza kama itakavyoonekana inafaa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za Baraza;

(k) kuanzisha kamati ikiwa ni miongoni mwa wajumbe wake au vyenginevyo, ambayo itakasimiwa uwezo huo kama itakavyoonekana inafaa;

(l) kuthibitisha mpango kazi na malengo ya Kamati na kusimamia maendeleo yake kwa ajili ya kufikia malengo endelevu; na

(m) kutekeleza jukumu jengine lolote watakalopewa chini ya Sheria hii au maelekezo ya Baraza.

Mkutano wa Kamati Tendaji.

**17.** Mkutano, akidi na maazimio ya Kamati Tendaji yatafanywa kama ilivyoelezwa katika Jadweli la Pili la Sheria hii.

## SEHEMU YA NNE
## UANZISHWAJI WA KAMATI ZA BARAZA

Kamati za Baraza.

**18.**-(1) Kutakuwa na Kamati zitakazoanzishwa na Baraza kama itavyoona inafaa.

(2) Kamati zilizoanzishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, zitakuwa na uwezo wa kushughulikia jambo lolote watakalopewa na Baraza, Taasisi ya kibiashara ya kijamii au mtu yeyote mwenye maslahi nalo.

(3) Baraza litakuwa na Kamati zifuatazo:

(a) Kamati ya Uchumi, Biashara, Uwekezaji na Kodi;

(b) Kamati ya Utalii;

(c) Kamati ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Mazingira; na

(d) Kamati ya mambo ya Ajira.

(4) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, Baraza linaweza kuanzisha au kuondosha Kamati nyengine yoyote kama itavyoona inafaa kwa utekelezaji wa kazi zake chini ya Sheria hii.

(5) Wajumbe wa Kamati zilizoanzishwa chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, watakuwa kama ilivyoainishwa chini ya Jadweli la Tatu la Sheria hii.

(6) Kwa kuzingatia miongozo na maelekezo yatakayotolewa na Baraza, Kamati zinaweza kuweka utaratibu wa uendeshaji wa shughuli zake zenyewe.

Kumualika mtu.

**19.** Kamati zinaweza kumualika mtu yeyote mwenye utaalamu mahsusi kuhudhuria na kushiriki katika majadiliano ya kamati kwa ajili ya kutoa ushauri kwa kamati hiyo juu ya jambo lolote lililojadiliwa.

Kazi za Kamati.

**20.**-(1) Kila Kamati ya Baraza itakuwa na kazi zake kama ifuatavyo:

(a) Kamati ya Uchumi, Biashara, Uwekezaji na Kodi ina wajibu wa:

(i) kuwezesha utekelezaji wa maazimio ya Baraza au Jukwaa la Biashara;

(ii) kupokea jambo lolote au lalamiko linalohusiana na biashara kutoka kwa mtu yeyote kwa mazingatio;

(iii) kutoa ushauri juu ya mambo mbalimbali yatakayosaidia kukuza uchumi endelevu;

(iv) kupendekeza namna ya kuimarisha mazingira mazuri ya kibiashara, viwanda na uwekezaji;

(v) kutatua matatizo yanayoikabili sekta ya biashara, viwanda na uwekezaji;

(vi) Kuimarisha ukusanyaji wa kodi na mapato;

(vii) kuainisha matatizo yanayoukabili mfumo wa kodi na kuyatatua;

(viii) kuimarisha fursa za uwekezaji kwa mashirikiano ya sekta ya umma na sekta binafsi; na

(ix) kutekeleza jambo jengine lolote watakaloelekezwa na Baraza.

(b) Kamati ya Utalii ina wajibu wa:

(i) kutoa ushauri juu ya mambo mbalimbali yatakayosaidia kukuza sekta ya utalii;

(ii) kuainisha matatizo yanayoikabili Sekta ya Utalii-Zanzibar;

(iii) kupendekeza hatua za kutatua matatizo ya sekta ya utalii;

(iv) kupendekeza hatua za kuimarisha sekta ya utalii;

(v) kuwezesha utekelezaji wa Baraza; na

(vi) kutekeleza jambo jengine lolote watakaoelekezwa na Baraza.

(c) Kamati ya Kilimo, Ufugaji, Uvuvi na Mazingira ina wajibu wa:

(i) kutoa ushauri juu ya mambo mbalimbali yanayohusiana na maendeleo katika Sekta ya Kilimo, Ufugaji, Uvuvi na Mazingira;

(ii) kuainisha matatizo yanayoikabili Sekta ya Kilimo, Ufugaji, Uvuvi na Mazingira;

(iii) kupendekeza hatua za kutatua matatizo yote katika Sekta ya Kilimo, Ufugaji, Uvuvi na Mazingira;

(iv) kuwezesha utekelezaji wa maazimio ya Baraza; na

(v) kutekeleza jambo jengine lolote watakaoelekezwa na Baraza.

(d) Kamati ya Ajira ina wajibu wa:

(i) kuanisha fursa za ajira;

(ii) Kutatua matatizo ya waajiri na wafanyakazi;

(iii) kuainisha matatizo yanayohusu ajira na kupendekeza hatua za kuyatatua;

(iv) kuwezesha utekelezaji wa maazimio ya Baraza; na

(v) Kutekeleza jambo jengine lolote watakaoelekezwa na Baraza.

(2) Baraza linaweza kuongeza au kubadilisha idadi ya kamati au wajumbe wa kamati hizo, pale itakapoona inafaa.

(3) Katibu Mtendaji atakuwa ni Katibu wa Kamati za Baraza isipokuwa anaweza kukasimu madaraka hayo kwa Afisa mwengine pale itakapohitajika.

(4) Katibu Mkuu Kiongozi atawajuilisha kwa maandishi wajumbe watakaoteuliwa kuwa wajumbe wa kamati mbalimbali.

(5) Kamati zitawasilisha taarifa za utekelezaji kwa ajili ya kuidhinishwa kama itakavyohitajika na Baraza ndani ya muda utakaoamuliwa na Kamati Tendaji.

(6) Ukitoa wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, Wajumbe kutoka Sekta binafsi watashikilia nafasi kwa kipindi cha miaka mitano na watakuwa na sifa ya kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YANAYOHUSIANA NA MABARAZA YA MIKOA

Muundo wa Baraza la Mkoa.

**21.**-(1) Kutakuwa na Baraza la Mkoa kwa kila Mkoa ambalo litakuwa na wajibu wa kutekeleza kazi za Baraza zilizokasimiwa kwa Baraza la Mkoa husika.

(2) Mkuu wa Mkoa wa Mkoa husika atakuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mkoa.

(3) Baraza la Mkoa linaundwa na wajumbe kumi na mbili, sita kutoka sekta ya umma na sita kutoka sekta binafsi.

(4) Wajumbe wa Baraza la Mkoa kutoka sekta ya umma watateuliwa na Mkuu wa Mkoa kwa kushauriana na Taasisi za umma husika.

(5) Wajumbe wa Baraza la Mkoa kutoka sekta binafsi wataeuliwa na Mkuu wa Mkoa kwa kushauriana na Taasisi binafsi katika Mkoa husika.

(6) Katibu Tawala wa Mkoa atakuwa Katibu wa Baraza la Mkoa.

Kazi za Baraza la Mkoa.

**22.** Baraza la Mkoa lina kazi zifuatazo:

(a) kutekeleza maazimio ya Baraza;

(b) kupeleka mapendekezo ya kibiashara kwa Baraza;

(c) kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa Baraza;

(d) kuwasiliana na Katibu Mtendaji kwa jambo lolote lililojitokeza linalohusiana na biashara kwa ajili ya kufanyiwa kazi na kulitatua;

(e) kuandaa jukwaa la majadiliano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi katika ngazi ya Mkoa;

(f) kupokea na kuzingatia mambo yote yanayohusiana na ukuzaji wa biashara na maendeleo ya uchumi katika ngazi ya Mkoa na kupendekeza njia muafaka;

(g) kujadili na kutafuta suluhisho la vikwazo vinavyohusiana na maendeleo ya biashara katika ngazi ya Mkoa; na

(h) kutekeleza jambo jengine lolote kama watakavyoelekezwa na Baraza.

Wajibu wa Baraza la Mkoa.

**23.**-(1) Baraza la Mkoa lina wajibu wa kusaidia utekelezaji wa kazi za Baraza katika ngazi husika ya Mkoa kwa ajili ya kuhakikisha jukwaa la majadiliano kuhusiana na masuali ya biashara baina ya Serikali na sekta binafsi linafanikiwa.

(2) Baraza la Mkoa litatekeleza kazi zake chini ya usimamizi na maelekezo ya Baraza.

(3) Baraza la Mkoa litakutana katika vikao vyake vya kawaida mara mbili kwa mwaka, lakini linaweza kuitisha kikao cha dharura wakati wowote kadri hali itakapohitajika.

(4) Baraza la Mkoa linaweza kuanzisha kamati mbali mbali za kutekeleza kazi, pale itakapoona inafaa, kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa kazi za Baraza katika ngazi ya Mkoa husika.

(5) Baraza la Mkoa litaweka na kuhifadhi kumbukumbu za kila kikao na litatayarisha ripoti ya utekelezaji ya mwaka na kuiwasilisha kwa Kamati Tendaji ya Baraza na ripoti hiyo ya mwaka itajumuisha:

(a) utekelezaji wa kazi na shughuli za Baraza la Mkoa;

(b) utekelezaji wa maelekezo ya Baraza;

(c) mapato na matumizi;

(d) mapendekezo juu ya kuimarisha maendeleo ya biashara katika ngazi ya Mkoa husika; na

(e) utekelezaji wa kazi nyengine yoyote inayohusiana na biashara katika ngazi ya Mkoa.

(6) Vyanzo vya fedha vya Baraza la Mkoa vitatoka Baraza la Taifa la Biashara.

## SEHEMU YA SITA
## UANZISHWAJI WA JUKWAA LA BIASHARA

Kuanzishwa kwa Jukwaa la Biashara.

**24.**-(1) Kutakuwa na Jukwaa la Biashara la Baraza ambalo litakuwa na muundo ufuatao:

(a) Mwenyekiti wa Baraza ambae atakuwa Mwenyekiti;

(b) Wajumbe wa Baraza;

(c) Wajumbe wa Baraza la Mkoa;

(d) Wajumbe kutoka Jumuiya ya Wafanyabiashara;

(e) Wajumbe kutoka jumuiya nyengine za kibiashara; na

(f) Wafanyabiashara wengine kama Baraza litakavyoamua.

(2) Baraza litaandaa Jukwaa la biashara baina ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa ajili ya kukuza mashirikiano na majadiliano.

(3) Jukwaa la biashara litafanywa mara moja kwa mwaka, lakini linaweza kufanyika itakapohitajika.

(4) Baraza linaweza kumwalika mtu yeyote kuhudhuria Jukwaa la biashara.

(5) Jukwaa la biashara litapokea, litajadili na kutoa mapendekezo juu ya mambo yaliyowasilishwa na Baraza.

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI YA FEDHA

Vyanzo vya fedha.

**25.** Kutakuwa na vyanzo vya fedha vya Baraza ambavyo vitajumuisha:

(a) Fedha zitakazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kwa madhumuni ya Baraza;

(b) michango kutoka sekta binafsi; na

(c) Fedha zilizopatikana kwa njia za halali ambazo zitalipwa au kuingizwa kwa Baraza chini ya masharti ya Sheria hii.

Makadirio ya mwaka.

**26.**-(1) Angalau miezi mitatu kabla ya kuanza kwa kila mwaka wa fedha, Katibu Mtendaji atatayarisha makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka ya Baraza kwa ajili ya mwaka unaofuata.

(2) Katibu Mtendaji kabla ya kuanza kwa kila mwaka wa fedha, atawasilisha kwa Kamati Tendaji makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka kwa ajili ya kuidhinishwa.

Hesabu na ukaguzi.

**27.**-(1) Baraza litalazimika kusimamia vitabu vya hesabu na kumbukumbu za risiti za matumizi.

(2) Vitabu vya hesabu na kumbukumbu za fedha za Baraza zitahifadhiwa kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na Kanuni zake.

(3) Vitabu vya hesabu vitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mtu mwengine yeyote aliyemuidhinisha miezi mitatu baada ya mwisho wa kila mwaka wa fedha.

(4) Hesabu zilizokaguliwa na ripoti ya Mkaguzi zitawasilishwa katika Baraza si chini ya miezi sita baada ya kumalizika mwaka wa fedha.

(5) Katibu Mtendaji analazimika baada ya kupokea ripoti kutoka kwa mkaguzi, kuiwasilisha kwa Kamati Tendaji.

(6) Katibu Mtendaji analazimika, kumpa taarifa zote Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa hesabu za Serikali na kumuwezesha kufanya ukaguzi.

(7) Katibu Mtendaji analazimika kuiwasilisha taarifa ya mwaka kuhusu usimamizi wa fedha kwa mwaka huo wa fedha, pamoja na maelezo ya fedha kwa Kamati Tendaji na Waziri kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

(8) Matumizi yoyote ya Baraza yatafanywa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na Kanuni zake.

## SEHEMU YA NANE
## MASHARTI MENGINEYO

Kanuni.

**28.** Waziri anaweza, kwa kushauriana na Kamati Tendaji, kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

Kufuta na kubakiza.

**29.**-(1) Tangazo la Kisheria Namba. 106 la 2011 linafutwa.

(2) Bila ya kujali ufutwaji wa Tangazo la Kisheria katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, jambo lolote lililofanywa au hatua yoyote iliyochukuliwa au iliyofanywa, litachukuliwa kwamba limefanywa au kutekelezwa chini ya masharti ya Sheria hii.

## JADWELI LA KWANZA

### UTARATIBU WA UENDESHAJI WA VIKAO VYA BARAZA
**[Chini ya Kifungu cha 10]**

Vikao vya Baraza.

**1.** Baraza litafanya vikao vyake mara moja kwa mwaka, lakini linaweza kufanya kikao chengine cha dharura wakati wowote, pale litakapoona inafaa.

Akidi.

**2.** Akidi ya vikao vya Baraza itakuwa zaidi ya nusu ya wajumbe wa Baraza na miongoni mwa wajumbe waliohudhuria, kila upande baina ya sekta ya umma na sekta binafsi utapaswa kuwakilishwa na angalau asilimia arubaini ya wajumbe waliohudhuria.

Uendeshaji wa Vikao.

**3.** Vikao vyote vya Baraza vitaongozwa na Mwenyekiti.

Maazimio kuhusu jambo la dharura.

**4.**-(1) Endapo kwa maoni ya Mwenyekiti, ikiwa kuna jambo linaonekana ni la haraka na la dharura na haliwezi kusubiri utaratibu wa kuja kujadiliwa katika vikao vya Baraza, jambo hilo linaweza kujadiliwa na kutolewa maazimio katika ngazi ya kamati.

(2) Maazimio yaliyofikiwa chini ya kifungu cha 4(1) cha Jadweli hili, yatakuwa ni halali na yenye nguvu na yatatolewa ufafanuzi na itawasilishwa taarifa yake katika Baraza kwa ajili ya mazingatio na kuthibitishwa.

Maazimio ya pamoja.

**5.** Maazimio ya Baraza kwa jambo lolote lililoletwa kwa kufanyiwa maazimio yatafanywa kwa kufikia maazimio ya pamoja.

## JADWELI LA PILI

## UTARATIBU WA UENDESHAJI VIKAO VYA KAMATI TENDAJI
**[Chini ya Kifungu cha 17]**

Vikao vya Kamati Tendaji.

**1.** Kamati Tendaji itafanya vikao vyake vya kawaida mara mbili kwa mwaka na inaweza kufanya kikao cha dharura wakati wowote pale inapohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake sehemu yoyote kama itakavyoamuliwa na Kamati Tendaji.

Uendeshaji wa Vikao.

**2.** Vikao vyote vya Kamati Tendaji vitaendeshwa na Mwenyekiti na ikiwa Mwenyekiti hayupo, Mwenyekiti Mwenza kutoka Jumuiya ataendesha kikao hicho.

Mwenyekiti Mwenza.

**3.** Wajumbe wa Kamati Tendaji watamteuwa mjumbe mmoja miongoni mwao kuwa Mwenyekiti Mwenza.

Akidi.

**4.** Akidi ya vikao vya Kamati Tendaji itapatikana kwa zaidi ya nusu ya wajumbe wake kutoka sekta ya umma na sekta binafsi.

Maazimio ya pamoja.

**5.** Maazimio ya Kamati Tendaji yatapatikana kwa maridhiano ya wajumbe waliohudhuria kikao.

**JADWELI LA TATU**

**WAJUMBE WA KAMATI ZA BARAZA**
**[Chini ya kifungu cha 18(5)]**

**1.** Muundo wa wajumbe wa Kamati utakuwa kama ifuatavyo:

(a) Wajumbe wa Kamati ya Uchumi, Biashara, Uwekezaji na Kodi:

(i) Waziri mwenye dhamana na Biashara ambaye ni Mwenyekiti;

(ii) Waziri mwenye dhamana ya Fedha;

(iii) Waziri mwenye dhamana ya Ardhi;

(iv) Waziri kutoka Afisi ya Makamu wa Pili;

(v) Katibu Mkuu, kutoka Wizara yenye dhamana ya Biashara;

(vi) Katibu Mkuu, kutoka Wizara yenye dhamana ya Fedha;

(vii) Rais kutoka Jumuiya wa Wafanyabiashara, wenye Viwanda na Wakulima;

(viii) Mfanyabiashara maarufu atakayeteuliwa na Jukwaa la Wafanyabiashara;

(ix) Katibu Mtendaji kutoka Tume ya Mipango;

(x) Mkurugenzi Mtendaji kutoka Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi Zanzibar;

(xi) Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania;

(xii) Kamishna wa Bodi ya Mapato Zanzibar;

(xiii) Mjumbe kutoka jumuiya ya usafirishaji na utoaji mizigo; na

(xiv) Mjumbe kutoka Skuli ya Usimamizi wa Fedha (ZIFA) ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar.

(b) Wajumbe wa Kamati ya Utalii:

(i) Waziri mwenye dhamana ya Utalii ambaye ni Mwenyekiti;

(ii) Waziri mwenye dhamana ya Mawasiliano na Miundombinu;

(iii) Waziri mwenye dhamana ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa;

(iv) Waziri kutoka Afisi ya Makamu wa Pili;

(v) Katibu Mkuu, Wizara yenye dhamana ya Ardhi;

(vi) Katibu Mkuu, Wizara yenye dhamana ya Utalii;

(vii) Katibu Mtendaji Kamisheni ya Utalii;

(viii) Mkurugenzi Mtendaji kutoka Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi Zanzibar;

(ix) Mjumbe kutoka Jumuiya ya Wawekezaji wa Sekta ya Utalii;

(x) Mjumbe kutoka Jumuiya ya wanaotembeza watalii. na

(xi) Mjumbe kutoka Skuli ya Maendeleo ya Utalii ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar.

(c) Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Ufugaji, Uvuvi na Mazingira:

(i) Waziri mwenye dhamana ya Kilimo ambaye ni Mwenyekiti;

(ii) Waziri mwenye dhamana ya Biashara;

(iii) Waziri mwenye dhamana ya Ardhi;

(iv) Katibu Mkuu, Wizara yenye dhamana ya Kilimo;

(v) Mjumbe kutoka Jumuiya ya Wakulima wa Mikarafuu;

(vi) Mjumbe kutoka Jumuiya wa Wafanyabiashara, wenye Viwanda na Wakulima;

(vii) Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar;

(viii) Mjumbe kutoka Chama cha Wakulima wa Matunda na Mboga Zanzibar;

(ix) Mjumbe kutoka Chama cha Wafugaji Zanzibar;

(x) Mjumbe kutoka sekta ya Mazingira; na

(xi) Mjumbe kutoka sekta ya uvuvi.

(d) Wajumbe wa Kamati ya masuali yanayohusiana na Ajira:

(i) Waziri mwenye dhamana ya Ajira ambaye ni Mwenyekiti;

(ii) Waziri mwenye dhamana ya Utumishi wa Umma;

(iii) Katibu Mkuu, Wizara yenye dhamana ya Kazi;

(iv) Katibu Mkuu, Wizara yenye dhamana ya Utumishi wa Umma;

(v) Mjumbe kutoka Chama cha Wakandarasi;

(vi) Kamishna wa Kazi;

(vii) Kamishina wa Uhamiaji Zanzibar;

(viii) Mjumbe kutoka Chama cha Waajiri Zanzibar;

(ix) Mjumbe kutoka Chama cha Wafanyakazi Zanzibar;

(x) Mkuu wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali; na

(xi) Mjumbe kutoka Chuo cha Utawala wa Umma (IPA).

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 28 Septemba, 2017.

.................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi***

***Zanzibar***